



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



TAARIFA KWA UMMA

KUHUSU UTEUZI WA DIWANI WA VITI MAALUM

Kwa kuzingatia matakwa ya kifungu cha 86A cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, Tume ya Taifa ya Uchaguzi katika Kikao chake cha tarehe 19 Mei, 2018, imemteua Ndugu **FATUMA SALUM NGOZI** kuwa Diwani wa Viti Maalum katika Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara Mikindani kupitia Chama Cha Wananchi (CUF).

Uteuzi huu umefanyika baada ya kupokea taarifa kutoka kwa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa ambaye kwa mujibu wa kifungu cha 13 (1) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, aliitaarifu Tume ya Taifa ya Uchaguzi uwepo wa nafasi hiyo wazi. Tume baada ya kupokea Taarifa hiyo, ilikifahamisha Chama Cha Wananchi (CUF), ambacho kiliwasilisha jina la anayependekezwa kuteuliwa kuwa Diwani wa Viti Maalum kutoka katika orodha ya majina yaliyowasilishwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi mwaka 2015.

Imetolewa na:


Kailima, R. K

MKURUGENZI WA UCHAGUZI

19 Mei, 2018